

OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI KIFARU

SIMU 0677- 470322

KUMB.NA KHS/VOL.I/ FOEF/2016.

KIDATO CHA : TANO

TAREHE :.....

MZAZI/ MLEZI :.....

S. L. P.

YAH: MAELEKEZO NA MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE.

A. Utangulizi

1. Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Kifaru kidato cha TANO Mchepuo wa
2. Uongozi wa Shule unachukua nafasi hii kukupongeza na kukukaribisha . Aidha tunaamini kuwa wakati wote utakaokaa KIFARU utazifanya shughuli zote za kielimu kwa juhudi , maarifa na uadilifu ili kiwango cha ubora wa Elimu Shuleni hapa .
3. Kifaru ni Shule ya kutwa kwa wanafunzi wa kidato cha I hadi cha IV, baadhi ya wanafunzi wanakaa hosteli, na bweni ni kidato cha V na VI.
4. Shule hii iko kilometa 1¹/₂ kusini mwa barabara kuu ya Moshi – Dar es salaam unaweza kushukia kwenye kibao cha Shule ya Sekondari Kifaru au Stendi ya mabasi Kifaru.
5. Shule itafunguliwa kwa muhula wa kwanza tarehe Unapaswa ufike shuleni mapema iwezekanavyo, muda usizidi saa 11:00 jioni ili upokelewe na kukabidhi vitu ulivyoagizwa.

B. Tafadhali zingatia kujaza na kurudisha fomu muhimu kama ifuatavyo.

- i) Fomu ya mapokezi na utambulisho
- ii) Fomu ya uthibitisho wa afya yako (Medical examination form) isainiwe na daktari wa Wilaya.
- iii) Fomu maalum ya wageni
- iv) Hati ya utii na sheria.

C. Mzazi mwandalie mwanao mahitaji yafuatayo.

- i) Godoro la sponji futi 2.5 upana (Ujinunulie / uje nalo)
- ii) Shuka 2 rangi ya kijani kibichi, mto na foronya.
- iii) Sanduku la bati kwa usalama wa vifaa vyake
- iv) Taalo, sabuni, mswaki na dawa, rangi ya viatu, tochi na chandarua
- v) Vitabu vya sala – kulingana na dhehebu lake.
- vi) Sahani, kijiko, bakuli na kikombe.

D. Vifaa vyake vya Taaluma .

- i) Daftari 8 kubwa , kalamu ya bluu au nyeusi , pensili na rula.
- ii) Cofa/ kebe (Mathematical Instruments set).
- iii) Four figure table (Logarithm table) kwa wanaosoma hesabu.
- iv) English dictionary (Kamusi ya Kiingereza) na vitabu vingine vya kiingereza (kwa wanaosoma kiingereza).
- v) Kamusi ya Kiswahili na vitabu vya Kiswahili (kwa wanaosoma Kiswahili)
- vi) Vitabu vya Geography (kwa wanaosoma Geography)
- vii) Vitabu vya History (kwa wanaosoma History)
- viii) Vitabu vya Economics (kwa wanaosoma Economics)
- ix) Vitabu vya Bam (kwa wanaosoma Bam)
- x) Vitabu vya Advanced mathematics (kwa wanasoma EGM)
- xi) Calculator (Non programmable)

I. MAHITAJI.

a) ADA NA MICHANGO YA SHULE.

NA.	MCHANGO KWA MWAKA	KIASI CHA TSH.
1	Ada	70,000/=
2	Tahadhari	5,000/=
3	Huduma ya Afya / Matibabu	10,000/=
4	Matron / Patron	15,000/=
5	Ulinzi	10,000/=
6	Uboreshaji taaluma	20,000/=
7	Wapishi	5,000/=
8	Ukarabati	20,000/=
	Jumla	155,000/=

Weka fedha hizo katika akaunti ya Shule Na. 4021100020 NMB Kifaru Sekondari na kisha ulete risiti kutoka benki uliyolipia malipo hayo Shuleni. Andika jina la mwanafunzi na kidato chake katika risiti hiyo.

Mwanafunzi awe amelipa Ada ili aweze kupokelewa.

Ada na michango mingine ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taaluma hapa shuleni , hivyo mzazi hakikisha umemlipia mwanao ada na michango mingine.

MUHIMU: (i) Kwa wale watakaolipiwa na Halmashauri wakumbuke kuleta barua za kuwatambulisha .

(ii) Kila mwanafunzi aje na Tsh. 15,000/= kwa ajili ya dawati, Tsh, 7,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha za passport size .

(iii) Kila Mwanafunzi aje na result slip ya matokeo ya kidato cha nne na living certificate (cheti halisi na vivuli vyake (Photocopy)

SARE ZA SHULE.

Wavulana.

- Suruali mbili (2) @ sh 18,000 = 36,000/= (Zinashonewa shuleni za rangi ya kijivu)
- Suruali mbili (2) @ sh 18,000/= 36,000/= rangi nyeusi za kushindia pia zitashonwa shuleni kwa muundo uliopangwa.
- T-shirt za kushindia nyeupe na bluu zenye nembo ya shule zinapatikana shuleni kwa Tshs. 10,000/= kila moja.
- Sweta 1 sh. 15,000/= zinapatikana shuleni kwa atakayehitaji.
- Shati mbili nyeupe za mikono mifupi aje nazo
- Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi
- Soksi jozi 2 nyeusi aje nazo
- Aje na sare ya shule alikotoka kidato cha nne na atavaa kwa muda hadi atakapo shonewa nyingine.

Wasichana.

- Sketi 2 @ 18,000/= 36,000/= (Zitashonewa shuleni za rangi ya kijivu)
- Soksi jozi 2 nyeupe aje nazo
- Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba visigino vifupi aje nazo
- Sketi mbili za kushindia @ 18,000/= 36,000/= (Zinashonewa shuleni)
- T-shirt za kushindia nyeupe na bluu zenye nembo ya shule zinapatikana shuleni kwa Tshs. 10,000/= kila moja.
- Sweta 1 sh. 15,000/= zinapatikana shuleni kwa atakayehitaji
- Shati mbili nyeupe za mikono mifupi zenye vifungo vya kawaida aje nazo
- Aje na sare ya shule alikotoka kidato cha nne na atavaa kwa muda hadi atakapo shonewa nyingine.

VIFAA VYA KAZI NA MICHEZO.

A. WASICHANA

- Raba jozi moja (Nyeusi)
- Bukta ya michezo rangi ya bluu na T – sheti ya bluu isiyo na maandishi wala michoro yeyote.
- Ndoo za plastiki 2
- Jembe lenye mpini
- Reki yenye mpini
- Hard broom – wasichana.

B. WAVULANA

- Raba jozi moja (Nyeusi)
- Bukta ya michezo rangi ya bluu na T – sheti ya bluu isiyo na maandishi wala michoro yeyote.
- Ndoo za plastiki 2
- Fagio la chelewa refu lenye mpini
- Panga / kwanja.
- Squezer (Mopper)

NB. Tafadhali zingatia kifaa ulichoagizwa .

MAAGIZO.

- i) Kila mwanafunzi lazima asome sheria , kanuni na taratibu za shule kwa uangalifu azifuata na kuzitii . Kutofanya hivyo ni makosa.
- ii) Uvunjaji wa sheria yoyote ya shule hata ikiwa ndogo kiasi gani hautavumiliwa
- iii) Mwanafunzi lazima ahudhuria vipindi vyote na afanye mazoezi na mitihani ya masomo yote yanayofundishwa darasani kwake. Ni kosa linaloweza kumfukuzisha mwanafunzi shuleni kwa kuacha kuhudhuria vipindi na kuacha kufanya mazoezi / mitihani bila sababu za msingi.

I. SHERIA ZA BWENI.

- i) Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuchemsha/ kupika bwenini aidha kwa kutumia moto wa kuni, mkaa , mafuta ya taa au moto wa umeme.
- ii) Bwenini ni mahali pa kulala si pa kupiga kelele. Usemi wa bwenini uwe mazungumzo ya maana ya sauti ndogo . Upigaji kelele au mayowe ni dalili za ulevi , uhuni, fujo, n.k. hiyo haikubaliki.
- iii) Usafi wa bweni ndani na nje (mazingira yanayozunguka bweni ni wajibu wa kila mkaaji wa bweni husika)
- iv) Ni makosa kukaribisha mgeni wa aina yoyote bwenini au katika eneo la bweni
- v) Vyoo vyote lazima vitumike vizuri na kuwekwa katika hali ya usafi
- vi) Ni wajibu wa viongozi wa bweni pamoja na wana – bweni wote kulinda sheria kwa kuzitekeleza kwa vitendo.
- vii) Mwanafunzi haruhusiwi kuja shuleni na vyombo vifuatavyo:- Redio , pasi, Heater, Kamera . Simu ya mkononi , Hot pot, Walk man au kifaa chochote cha muziki , Sufuria , Pombe , Madawa ya kulevya

NB: Mwanafunzi atakayekutwa na vitu tajwa hapo juu atachukuliwa hatua kali. Unaweza kuja chupa ndogo ya chai (Thermos)

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA NI.

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
5. Kpigana au kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito/ kupata mimba.
9. Kuoa na kuolewa
10. Kusababisha mimba
11. Kutoa mimba.
12. Makosa ya jinai
13. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
14. Kukataa adhabu kwa makusudi.
15. Kuwa na simu ya mkononi.

ADHABU:

Mwanafunzi yeyote atakayevunja sheria za shule ataadhibiwa mara moja na asipojirekebisha atafukuzwa shule.

.....
MKUU WA SHULE.

III. MAAGIZO KWA WAZAZI.

Sheria za shule zimeorodheshwa . Wazazi na wanafunzi ni muhimu kusoma kwa uangalifu na kutia saina zenu za makubaliano katika fomu ya HATI YA UTII NA SHERIA ambayo imeambatanishwa halafu irudishwe kwa Mkuu wa Shule. Ni dhahiri kuwa wanafunzi watakuwa wamepoteza wakati wao bure kama wasipotaka kufanya kazi zote kwa bidii na kutii sheria za shule .

i) Wazazi / wageni kutembelea shule.

Wazazi hawaruhusiwi kuwatembelea watoto wao kwa tarehe zisizostahili . Baadhi ya wazazi wamekuwa na tabia ya kufika shule na kutaka kuwaona watoto kwa tarehe zisizostahili . Unaruhusiwa kumtembelea mwanao Jumamosi/ Jumapili ya mwisho ya kila mwezi

ii) Wanafunzi kutembelea nyumbani .

Mwanafunzi haruhusiwi kwenda nyumbani isipokuwa

- a) Ametumwa / amepolekwa na shule.
- b) Wazazi wake waje kumchukua kukitokea shida kubwa nyumbani mfano. Msiba , Ni lazima waje na barua yenye saina na muhuri wa mtendaji wa Kijiji kuthibitisha tukio hilo.
- c) Mapumziko mafupi ya katikati ya muhula (Mid term break) au likizo ndefu.

iii) Tiba

Mwanafunzi haruhusiwi kuja na dawa zake binafsi kwani atahudumiwa katika zahanati ya shule, lakini ikiwa amepewa dawa na Daktari atamkabidhi muuguzi wa shule ambaye atafuatilia matumizi yake.

iv) Chakula

Shule inajitahidi kuwapa wanafunzi chakula bora na cha kutosha . Mwanafunzi haruhusiwi kuleta chakula cha aina yeyote shuleni . Wanafunzi wanaruhusiwa kujinunuliwa vitafunwa katika kantini ya shule au duka la shule siku za mahafali shule inatengeneza chakula “special “ kwa ajili ya wahusika wote. Wazazi hawaruhusiwi kuingiza chakula wala kinywaji chochote shuleni . Mzazi haruhusiwi kuingiza zawadi yoyote shuleni .Zawadi hazitapokelewa wawekeeni watoto wenu muwakabidhi warudipo nyumbani.

v) Pesa za matumizi.

Ni wazi kuwa mwanafunzi lazima apewe pesa za matumizi . Ni wajibu wa mzazi / mlezi kumpa mtoto kiasi cha pesa anunue sabuni, stampu, bahasha, na vitu vingine vidogo. Kuna wazazi wengine wanawapa watoto wao pesa nyingi mno mpaka inashangaza . Hivi ni kumzoeshwa mtoto vibaya , husababisha wizi, mashindano, ubaguzi, tabaka, ugomvi, na urafiki usio na msingi . Siyo busara kumpa mtoto fedha nyingi mno.

vi) Wajibu wa mwanafunzi awapo shuleni.

- a) Kutii sheria zote za shule
- b) Kuhudhuria vipindi vyote vilivyopangwa kwenye ratiba , kufanya mazoezi yote atakayopewa na mwalimu na kujisomea kwa bidii.
- c) Kushiriki shughuli zote za usafi, utunzaji wa mazingira ya shule , bustani na miradi mingine ya shule.

Hitimisho.

Wazazi tunaomba sana tuwe na malezi ya pamoja ili watoto wetu waendeleo na wapate kile walichokifuata hapa shuleni Kifarua yaani ELIMU . Msisitizo wa Bodi ya Shule ni kwamba kila mwanafunzi anatakiwa kusoma kwa bidii na kufaulu kwa kiwango cha alama 50% au zaidi katika kila somo. Sheria zote hizi zinalinga katika kumfanya mtoto apate mazingira bora ya kujisomea na hatimaye aweze kufaulu vizuri masomo yake.

TUNATEGEMEA USHIRIKIANO WAKO.

.....
MKUU WA SHULE.

MFOMU YA MAPOKEZI SHULENI
MAELEZO KUHUSU MWANAFUNZI (IRUDISHWE SHULENI)

SEHEMU: “A” – Ijazwe na mwanafunzi;

Jina la Mwanafunzi (majina matatu)

.....

Anwani;

Taifa / Uraia :

Dini :

Tarehe ya kuzaliwa :..... Jinsia :.....

Shule anakotoka (Shule ya Sekondari) :.....Kata ya

Mwaka wa kumaliza kidato cha nne :

Wilaya anakotoka :.....

Mkoa :.....

SEHEMU “B” (Ijazwe na mzazi/ mlezi)

Jina la mzazi / mlezi (majina matatu)

.....

Anwani ya mzazi/ mlezi :.....

Namba ya simu ya simu ya mzazi / mlezi.....

Mahali anapoishi :

Kazi ya mzazi / mlezi.....

Mahali anapofanya kazi :

Ndugu wawili wa karibu (wanaoweza kushika nafasi ya mzazi / mlezi)

- | | | |
|-----|-------|------------|
| i) | | Simu |
| ii) | | Simu |

SEHEMU “C”

- Tafadhali fika na vifaa vyote ulivyoagizwa
- Wahi shuleni kabla ya saa 11:00 jioni
- Mzazi hakikisha unakamilisha malipo yote kabla ya kumleta mwanao shuleni .

.....

SAHIHI YA MKUU WA SHULE

.....

SAHIHI YA MZAZI/ MLEZI

TAREHE:...

FOMU MAALUM KWA AJILI YA WAGENI WA WANAFUNZI HAPA SHULENI
(IRUDISHWE SHULENI)

FORM NA. KHS/1/2014.

A. NDUGU MZAZI.

Kwa kuwa Mwanafunzi amekabidhiwa kwa walezi ambao ni walimu pamoja na wafanyakazi wa shule hii, tunaomba utuorodheshee majina ya jamaa wa karibu watatu tu ambao unaweza kuwatuma kuja kumwona kwa sababu maalum tu.

NA.	JINA	UHUSIANO	KAZI YAKE	MAHALI ATOKAPO	NA. YA SIMU
1					
2					
3					

Mtu mwingine zaidi ya hao waliotajwa hapo juu haruhusiwi / mpaka alete barua ya kumtambulisha .

Mzazi/ mgeni yeyote akija aonane kwanza na uongozi wa shule (Mwalimu wa zamu au mlinzi) na ndio watakaomwita mwanafunzi.

N.B. Mwanao akikutwa / akitoroka kwenda kwenye sehemu za starehe muda wowote atakuwa amujifukuza shule mwenyewe moja kwa moja
Kama mwanao akirudi nyumbani atakuonyesha kibali maalum cha kutoka shuleni chenye muhuri husika wa shule , utapewa usaini kabla ya kukirudisha.

B. Siku za kuwatembelea wanafunzi rasmi ni jumamosi na jumapili ya (mwisho) ya kila mwezi

C. Mimi mzazi wa Nakubaliana na yote yaliyoandikwa hapo juu.
Naahidi kushirikiana nanyi.
Nikikiuka taratibu hizo mwanangu achukuliwe hatua kali za kunidhamu.

.....
SAHIHI MKUU WA SHULE

.....
SAHIHI YA MZAZI /MLEZI

**OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**Shule ya Sekondari
Kifaru,
S. L. P. 163,
MWANGA.**

Tarehe:.....

HATI YA UTII NA SHERIA

**Mimi Mzazi / Mlezi wa
..... nimesoma kwa makini Sheria za Shule kama
zilivyoandikwa katika Maagizo kwa Wazazi na nazikubali Sheria hizo na
nitashirikiana na Shule kuona kuwa mwanangu anazizingatia kwa manufaa ya
Umma.**

**Mimi(majina ya mwanafunzi)
Nimesoma kwa makini Sheria za Shule kama zilivyoandikwa na ninazikubali
Sheria hizo. Naahidi kuwa nitazifuata na kuzitii nikijua kuwa naelimishwa na
Umma kwa manufaa ya Umma.**

**.....
SAINI YA MWANAFUNZI**

**.....
SAINI YA MZAZI**

TAREHE:.....TAREHE :

MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING.

KIFARU SECONDARY
SCHOOL.
P. O. BOX 163,
MWANGA.

DATE:.....

REF: NO. KHS/MEX/VOL.I/2016.

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM.
TO THE MEDICAL OFFICER,

.....
.....
.....

Please examine (Name of students) who has been
selected to join this school for his fitness as a student in the following (To be completed
by a medical officer)

1. Eye sight
2. Hearing.....
3. Limbs.....
4. SPECIMEN
 - i) Stool.....
 - ii) Urine.....
 - iii) Blood.....
 - iv) Neurosis.....
5. Asthma.....
6. Tuberculosis
7. Pregnancy
8. Other serious disease:-
 - i) Venereal disease.....
 - ii) Leprosy
 - iii) Epilepsy

MEDICAL CERTIFICATE:
(To be completed by a Medical Officer)

I have examined the above and consider him/ her to be physically fit / unfit as a student

.

Date: Signature:

Station : Designation:.....

NB: I request this form to be returned to the school in a sealed – envelop.

.....

THE HEADMASTER